

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

Tel. 025-2540035

FAX NO. 025-2540425



P. O. BOX. 320,
KYELA
MBEYA - TANZANIA.

KUMB NA.KDC/PRS/A//02/12

07/06/2017

TANGAZO LA ZABUNI ZABUNI NA. LGA/074/2017/2018/PREQ/01 KWA AJILI YA KUPATA WAZABUNI UTOAJI WA HUDUMA, VIFAA NA MAKANDARASI WA MAJENGO, BARABARA NA UMEME MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela anawatangazia wananchi wote wenye uwezo na sifa ya **kutoa huduma, kuuza/kusambaza vifaa na Makandarasi kwa kazi za ujenzi na umeme** kwa kipindi cha mwaka wa fedha Julai, 2017 hadi Juni 2018 kuomba Zabuni mbalimbali zilizochanganuliwa kwenye jedwali lifuatalo :

Lot Na.	AINA YA ZABUNI
	LGA/074/2017/2018/PREQ/02 ZABUNI ZA HUDUMA NA VIFAA
1	Uuuzaji wa madawa na vifaa tiba (medical supplies & equipments)
2	Matengenezo ya vifaa tiba
3	Uuzaji wa Gas (LP Gas, gesi ya Majokofu n.k
4	Uuzaji wa Samani za ofisi (Furniture & Fittings)
5	Uuzaji wa Dizeli , Petroli na Mafuta ya taa (supply of diesel,petrol and Kerosene)
6	Huduma ya Matangazo kwa njia ya Vipaza Sauti Kutoa huduma ya Ulinzi katika ofisi za Halmashauri na maeneo mengine
7	
8	Huduma ya Usafi wa Mazingira katika Hospitali ya Wilaya
	LGA/074/2017/2018/PREQ/W/03 MAKANDARASI (Shortlisting of Contractors [Civil, Building & electrical])
9	Makandarasi wa kazi za ujenzi wa barabara, majengo na umeme

MASHARTI YA MWOMBAJI:

1. Mwombaji lazima awe na leseni ya biashara, TIN, Hati ya Usajili na Ofisi inayotambulika.
2. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha, athibitishe kwa kuambatanisha '**Bank Statement**' ya miezi mitatu (3) iliyopita kutoka tarehe aliyoomba zabuni au '**audited Financial Statement**' ya miaka miwili ya karibuni.
3. '**Power of Attorney**' kwa Zabuni husika iambatanishwe kweye maombi ya zabuni.
4. **Ada ya maombi ya zabuni ni Tshs.50,000/= (Elfu Hamsini tu)** ambapo kiasi hicho kitalipwa na kukatiwa stakabadhi ya malipo ambayo itaambatanishwa katika barua ya maombi na fedha hizo hazitarudishwa.
5. Mwombaji awe na vitendea kazi vya kutosha kumudu vyema zabuni anayoomba.
6. Vitabu Vya zabuni na maelezo mengine vinapatikana Ofisi ya Katibu wa bodi ya zabuni, S.L.P.320, Kyela. Kuanzia saa 2.30 asubuhi mpaka saa 8.30 alasiri (Jumatatu – Ijumaa).
7. Maombi yawe na maelezo ya kina na viambatanisho husika (**Company Profile**) na kutumwa kwa:-

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P.320
KYELA.**

8. Mwombaji awe na Mashine ya **Electronic Fiscal Devise (EFD)** zinazotolewa na TRA kwa ajili ya kutolea risti za malipo.
9. Maombi yatakayoletwa kwa njia ya FAX, Telefax na Telegraphic system hayatapokelewa na kufunguliwa siku ya Ufunguzi.
10. Mwisho wa kupokea maombi ni **Jumatano 28 JUNI,2017saa 5.00 asubuhi** na zabuni zote kufunguliwa **Jumatano 28 JUNI,2017 saa 5.00 asubuhi** katika ukumbi wa mikutano Boman. Waombaji mnakaribishwa kuhudhuria ufunguzi kwa gharama zenu.

B. Semwaiko
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KYELA**